# 1: KUTO KUJITAMBUA

Nikizungumzia kutokujitambua kwa mtu sizungumzii kujifahamu, na niwachache wanaojijua (kujitambua), mtu anayejijua(jitambua) ni yule anayejua au kufahamu taarifa kamili (complete information) kuhusu yeye.

Je unajitambua?

Namna ya kujitambua , naweza kueleza kwa namna ifuatavyo, au namna ya kujitambua ni kama ifuatavyo,

## I [illegible] ?

Ni swali linaloonekana ni rahisi sana, na wengi huwa wanakurupuka kulijibu wakati wanapoulizwa, kwa kujua ni majibu sahihi, lakinin pia kwa kawaida ukilinganisha majibu utakayopewa kwa namnafulani huwa yana usahihi au yanafanana sana kiasi kwamba ni vigumu kutofautisha, kwa mfano wa manenonyenye matamshi yanayofanana lakini maana zinatofautiana kabisa.

Sasa rafikiyangu naomba uchukue angalau dakika moja ujiulize WEWE( MIMI NI NANI?), kisha fikiria majibu uliyoyapata baada ya kujihoji swali husika, na angalia akili yako inapokimbilia kisha utakuja kujisahihisha kwa vile nitakavyo kufundisha.

Kwaharaka akili yako ilikimbilia kujitambulisha kwa majina yako, lakini tukimzungumzia wewe halisi , tunazungumzia usemi unaosema “ MIMI NI ZAIDI YA JINA LANGU”, kwamba tukizungumzia wewe tunazungumzia kitu tofauti na jina lako. Mfano ukawa unatumia jina Gift au Zawadi, maana ya majina haya ni kitu anacho tolewa kwa mtu bila ya yeye kujua au baada ya kupewa ahadi. Hapo tunakuwa tumezungumzia jina lako wewe lina maanisha kitu gani wala hatujakuongelea wewe, kwa sababu jina limewekwa ili tuweze kuku trace kwa urahisi. Tukiuliza wewe ni nani tunataka kumjua yule wa ndani ambaye ndio wewe, ambaye huyo anajijua haswa kuwa ni nani.

Sasa ukijiuliza kuwa wewe ni nani, unatakiwa kujitafsiri kama yule wa ndani anavyojitambua, siku hizi tunajikuta tuna watu wengi au wanavyuo wengi wanaojiita wasomi na usomi wao wakiwa masomoni au nje ya masomo hawajitambui kuwa wao ni kina nani.

Nikizungumzia kuwa wewe ni nani? Tunatakiwa tukae tuzungumzie kile kitu unachokiweza natural bila ya kujifunza au kufundishwa na mtu yeyote, yaani umesoma, ukaishi na mama yako akakufunza vitu vingi, ukaishi na marafiki mkafanya vingi, ukatazama ndani ya jamii lakini katika yote uliyopata huko na ukayafanyia kazi, hujaona kama yamekufikisha mahali unataka au huoni kama yatakufikisha mahali unapopataka, yaani mahali ambapo moyo wako ukafika ukatulia au ukaridhika, au hujaona mtu aliye mbunifu kwenye eneo fulani kuzidi vile ambayvo unaona ubunifu fulani ukiufanya japo

bado hujafafanya kitu husika. Au kile kitu unaona hakika nikikifanya hiki ninauwezo nacho na nikifanya nitafanikiwa.

Basi hicho ndicho tunachoweza kukitafsiri kwamba ni wewe,au kwa maana nyingine naweza kusema kipaji au kipawa, ni kitu unachoweza kukifanya pasipo mafunzo au copy, na ukitazama hatima ya yule aliyeko ndani yako (ambaye ni wewe) unaona jinsi atakavyofanikiwa na kuwa mtu mkubwa  mbeleni na ni njia ya kufanya ili ufanikiwe, hapo hatuzungumzii jina lako.

Jina lako liko kwaajili ya kurahisisha traceability ya mtu husika, maana pasipomjina tungepata taabu sana, maana ingekuwa unamwita mtu nayeye anaona kwamba unamwita mtu mwingine, lakini kwa sababu hiyo majina yakawepo na wakati mwingine kwenye baadhi ya mashamba ya wanyama  huwa utakuta mpaka wanyama wanapewa majina au identity ya namba ili kurahisisha kwamba kwenye wakati unamwitaji mnyama fulani,ili kumpata mpaka umfuate aliko ndipo aje , lakini akipewa jina au akawa anaitwa kwa namba fulani huwa ukiita kwa jina au namba lazima atakuja hatakama alikuwa mbali, kwahiyo habari ya jina lisikubabaishe nakujua hakika unajitambua.

Mtaalamu mmoja alisema USIPOJUA WEWE NI NANI,WATU WATAKUAMBIA WEWE AMBAYE SIYE,  akimaanisha kwamba pale ambapo utashindwa kujitambua, watu wataanza kukufafanulia kuwa wewe ni fulani ambaye sio wewe, ambapo wanachuo wengi, huwa wanasumbuliwa na tatizo hili, na kuishi huku wakijitelekeza waowenyewe. Vile utakavyoambiwa na watu kuwa wewe ni nani, ni tofauti na vile wewe utakavyo jitambua kuwa wewe ni nani! ,  kwa maana ya kuishi nje ya njia yako na kutembea kwenye majani kuliko na nyoka, siafu, na wadudu wa kila aina huku umeiacha njia safi.

Ukiishi kama wewe (yani yule wa ndani) ni rahisi sana kuitengeneza forcus kwenye kituambacho wewe unakihitaji,na kipo ndani yako,au kile ambacho unakifanya, wakatimwingine unaweza ukawa unasoma corse ambayo huitaki na umeingia kusoma kwasababu wazazi wamekulazimisha kuisoma na haipo ndani yako, lakini kwa sababu tu unajitambua hautadharau mahali ulipo, na utakuwa namipango ya kukufanikisha(kumfanikisha) ambaye ni wewe kwa nja ya kuchukua ujuzi mahali ulipo.

Ukiamua kutumia kitu ambacho kiko ndani yako  wakati mwingine hauhitaji kupata elimu juu ya kitu ulichonacho, nitumie mfano wa wana muziki,ambapo kwenye wanamuziki kunaaina mbili.

MWANAMUZIKI MWENYE  TAARUMA YA MUZIKI.

Huyu ni mwanamuziki, lakini maraninyingi mtu wa namna hii huwa ni yule anayeishi nje ya yeye(yule wa ndani) kwa kuimba muziki lakini ni kama fursa kwa kusomea mambo ya muziki,huyu ni mtu anayehitajika kutumia gharama fulani ili kupata uwezo

wa kuimba, wakati mwingine akafeli pamoja na taaruma yake, na asifanikiwe katika kuimba muziki, au muziki wake kutokutoka na kujulikana na watu au muziki wake huko ku HIT, si kwamba wanakosea

Wanauwezo wa kupangilia sauti.

Wanapumzi ya kutosha kwenye kuimba.

Ni mahiri kwenye kutunga nyimbo nzuri.

Wanauwe zomzuri wa kwenda na noten mbalimbali.

MWANAMUZIKI MWENYE GIFT YA MUZIKI.

Huyu nimtu anaye ishi ndani yake( anaishi ambaye ni yeye) (kusudi lake kuwepo hapa duniani), ni mtu ambaye

Hana taaluma ya muziki. Hajatumia gharama yoyote kwenye kutaka ujuzi wa kuimba, lakini moja kwa moja anajua kupanga sauti.

Automatic anajua kupanda na mawimbi ya sauti.

Mtunzi mzuri wa nyimbo na mashairi mazuri ya muziki.

Nyimbo zake zinapotoka zina HIT.

Watu wakisikiliza kazi zake huzipokea vizuri na hupendwa.

Hukubalika na watu.

Wakati huohuo tukumbuke kwamba huyu mtu hajasomea mambo ya muziki,na hajalipa gharama yoyote kukipata alichonacho,lakini kwake ni automatic. Sasa tukimuuliza mtu huyu kuwa WEWE NI NANI? Ni halali kwakwe kujibu *mimi ni mwanamuziki*( anamtambulisha yule mtu wa ndani anaye tengeneza muziki na kumfanyia motivation ya kuimba huku akimwaminisha kuwa unaweza hakuna anayejua kuliko wewe) wakati mwingine kuchukua taaluma ya muziki kwake nikama nyongeza na kujua taaluma inaelezanini kuhusu muziki ili awe bora Zaidi. Na nikichukua mfano wa waimbaji wa nyimbo za injili Bahatu Bukuku,Jenipher Mgendi na wengine lukuki si wale walio kaa darasani wakajifunza muziki ndipo waingie kuimba isipokuwa ni walikuwa tayari kuishi kama wao( kuishi utu wao wa ndani\ kuishi kama wao ni kina nani!)

Nichukue mfano mzuri wa mwimbaji wa nyimbo za injiri za masifu na maabudu, Dr. Ipyana, anafahamika na wengi na nyimbo zake zinapendwa haswa na wengi na zinanguvu ndani yake, lakini kasomea udaktari wa binadamu na anaimba badara ya kukaa hospitali kutibu wagonjwa, ila sasa kwanini anaimba kwasababu anakipawa cha kuimba( yaani utu wake wa ndani ni mwimbaji na udaktari ni professional tu) akitaka kuingia kwenye ajira ataingia lakini, utu wake wa ndani umemtengenezea

maisha.( fuatilia histaria yake na uone ni jihudi gani anazifanya hapo alipo ili kujitengeneza awe zaidi ya pale alipo).

Niende kwa wale wasanii wa bongo kuna Diamond Platnamz, Harmonize,Rayvan, ni hawa wachache tu lakini ukiangalia ni watu wakubwa, lakini ni kitugani kilicho wafanya wawe ivyo? Ni ule utayari na kuwa na kiu ya kufikia kuishi uhalisia wao. Na ukiangalia historia zao si zile za kwenda kirahisi tu isipokuwa niwatu ambao waliamua kwelikweli, kuhakikisha wanafika hatua watakayo ishi kwenye uhalisia swao.

Mpaka hapo nafikiri utakuwa umeelewa nikizungumzia wewe ni nani, ( kama mpakahapa bado hujaelewa nakusihi usiendelee kusoma mbele, rudia kusoma ili uelewe vizuri, kisha uendelee, ninacho kitamani uelewe ninachokieleza lakini pia uelewe wewe ni nani!). na

sasa ukishaelewa hapo kaa na utathmini wewe ni nani!, hapa ukishajihoji ujielewe vema wewe ni nani, hapo naweza sema umejitambua.

Sasa ukishajitambua, ukajua kuwa wewe ni nani, unamaswali kadhaa ambayo unatakiwa kujihoji ili uweze kujitambua kwa upana Zaidi, maana kujijua kuwa wewe ni nani haitoshi, isipokuwa umeelewa mambo yafuatayo…

## NATAKIWA KUFANYA NINI?

Kiurahisi ni kwamba ukishajua kuwa wewe ni nani!, unaanza kujitambua au majibu yako yatakuambia ni kitu gani unatakiwa kufanya, kwa sababu pale jibu linapotoka ndipo unaanza kuhama kutoka kujifahamu na kuingia kwenye kujijua kuwa unatakiwa kufanya nini.

Ni mfano kwamba kabla hujaanza kuuza duka au hujaingia dukani ukaaanza kuuza duka, marazote kama ni duka la nguo,ukimtazama mtu anayeuza nguo ni mtu wa kurudia mavazi yaleyale mara kwa mara, unaanza kuleta complain yaani huyu anauza nguo nzuri lakini mavazi yake ni yaleyale kila mara, kama ni mamantilie, ana mwili dhaifu na mwili wake nimwembamba, unaleta complain mbona hanenepi na anauza chakula kizuri atakuwa mgonjwa huyu, yote hayo unaongea kwasababu bado hujajua ni majukumu gani anayafanya akiwa hapo! , lakini tukishakuchukua tukakupa majukumu hayo ,muda sipunde tutaanza kuona hali yako ni kama ya wale uliokuwa unaleta complain napengine ukawa na hali mbaya kuliko wao!

Sasa wanachuo wengi wanapogundua wapo kwenye course ambazo haziendani na uhalisia wao , huwa wanahama na kuanza kuishi nje ya wao,na kuacha kabisa uhalisia wao,lakini pia huwa wanaanza kufanya vitu nje ya masomo na kujiharibu kwa ujanja wa kijinga.

Nichukue mfano wangu mwenyewe bila kuumiza kichwa, mimi nimejitambua kuwa mimi ni mwalimu,nikiwa kidato cha tatu, wakatihuo nikiwa na ndoto za kuwa daktari, na

tukienda na mitaalayetu ya kielimu baada ya kumaliza kidato cha nne, nikachaguliwa kwenye course ya ANIMAL HEALTH AND PRODUCTION, sikusema kwasababu nina ndoto ya kuwa daktari wa binadamu sitoenda kusoma, japo ilitokea chance ya baba kutaka niende nikasomee nursing na application zikaanza lakini ikabidi application ighairishwe kwasababu nilikuwa na utayari wa kusomea afya ya mifugo na course nilikuwa nimeikubali kwawakati huo, nikaingia masomoni,huku nikiendelea kuchunguza,namna gani naweza kuwa daktari wa binadamu, kwa namna fulani nilipata taarifa za kunipa faraja kwamba naweza kutumia hii ngazi ya elimu niliyonayo kwenda kusomea pia afya ya binadamu, lakini pia nikifikia ngazi ya juu zaidi naweza ingia kwenye taasisi zinazohusika na afya ya binadamu, wakati huo ni ndoto hiyo na sijafikiria kwa habari ya uhalisia wangu ( kuwa mimi ni nani), na wakati naendelea na masomo nikafanya review kuwa mimi ni nani, baada ya hapo nikaanza kuyasoma mazingira ninayoishi na kuyachukua kama fursa ya kukitumia kitu kilichondani yangu, sikuridhika na namna elimu yangu nitaifikisha ili kukamilisha ndoto yangu, lakini nikagundua wakati nasoma natakiwa kuanza kumtengeneza yule ambaye ni mimi, bila kuangalia niko kwenye hali gani, ( nikajua natakiwa kufanya nini) na baada ya kujua natakiwa kufanya nini nikaanza utekelezaji na kuanza kuandika vitabu kama vitano vya kiimani nikafanikiwa kufungua kitabu kimoja, kinaenda kwa jina KUTAMBUA VITA ULIYONAYO ROHONI NA MBINU ZA KUPAMBANA (ni kitabu kizuri kama wewe ni mkrito unaweza ukakifuatilia ili ukipate kinamafunzo mazuri yatakayo kufanya upige hatua), haikuwarahisi lakini sikukata tamaa sababu napambana kumtengeneza yule mwandishi wa vitabu vizuri vya mafundisho ndani yangu na hamasa yake ni kubwa kiasi kwamba siwezi kumzuia na inabidi nitekeleze kile anacho niambia. Nilipomweleza baba mmoja kuhusu mimi na vitabu mbalimbali nilivyo viandaa, alishangaa sana na kuniuliza kwavile course yenu ni ngumu, unapata wapi muda wa kufanya yote haya?, nikamwambia nikiwa na mtengeneza yule ambaye ni mimi, siangalii ugumu wa mazingira niliyoko, niko tayari kutoa muda wangu ili nimkamilishe yule ambaye ni mimi. na huwa mwandishi( mwalimu) aliyeko ndani yangu ni mfuatiliaji mzuri wa kazi anazozitoa, na kuhakikisha kazi anazonipatia nafanya, na pale nisipotekeleza huwa adhabu pia napata ( kuto kuona raha kamili ya maisha, kukosa amani ya moyo kwenye kitu ninachokifanya nje ya maagizo) kwa hiyo baada ya kuona hayo nakaa kuomba msamaha kisha kuendelea na kazi aliyoniagiza ifanyike na isipofanyika haachi kunikumbusha.

Ni namna najaribu kukuelewesha namna gani mtu wa ndani( ambaye ni wewe) huwa anafanya kazi pale anapofahamu kuwa unajitambua na kuanza kutoa majukumu ya kitu gani ufanye, na kwa wakati gani, huwa anatoa direction ya maisha yako, la! Usipo jitambua huwa analala kabisa na kukuacha kabisa na kukuacha uishi maisha ambayo sio wewe ( uhalisia wako), ningeweza kukupa mengi anayonifundisha na kunifanyia lakini kwa haya machache nakupa ili upate mwanga kwamba huwa anafanya kazi namna gani!

Kwahiyo swali muhimu pia ni kujua ni nini unatakiwa kufanya, kisha kuanza kutekeleza kile kitu unachotakiwa kukifanya, maana kujua kuwa unatakiwa kufanya nini na usifanye ni heri usifahamu kabisa, kwahiyo nivyema kujua unatakiwa kufanya nini na ukafanya kwa uwezo ulionao kwasababu hujui ni lini utaibuka na kufanikiwa zaidi ya vile unawaza wewe, kuliko ukaacha na baadae ikatokea fursa ukaanza kulaumu, kwanini sikufanya!.

## KWA WAKATI HUU NAFANYA NINI?

Baada ya kujua unatakiwa kufanya kitu gani, your needed to ask yourself, what things am doing now, then compare to what your doing and what your needed to do.

Kile kitu unachokifanya je! kinaendana na wewe (yule wa ndani )?, au kwa namna gani kinaweza kumtengeneza ambaye ni wewe ( yule wa ndani ambaye ni uhalisia wako)?.

Wanavyuo wengi waliopo masomoni, wamekwama kwenye hili huku wakijua wapo kwenye usahihi wao (uhalisia wao) lakini kiuhalisia wako nje ya wao kwa kufanya vitu visivyo wahusu na havina uhusiano kabisa na utu wao wa ndani.

Wengi wanafanya vitu kwa mihemko, au kwa kuangalia wengine wanataka nini, bila kujali wao wanataka nini, nawahurumia vijana fulani ninao soma nao wanao fanya vitu vingi visivyosahihi kwa kuwachekesha watu ( hufanya vitu for leisure of others) na vingine kwa kuumiza watu na kujiona ni wajanja lakini wanasahau hao watu wanao wafanyia hivyo ndio wanaotakiwa kusimama mahali kama connection yao lakini sasa, ule wakati wao watakuwa na uhitaji wa kupata ajira wanaowafikiri kuwa ni connection zao ndio wanakumbuka maisha ya chuo jinsi yalivyokuwa wakiyaendesha, kunatokea maneno haya “hii nafasi naona angefaa fulani kuipata lakini kwa zile tabia zake hafai,( tayari mtu anakuwa amekosa kazi ambayo ingemfaa kabisa aipate na ilikuwa wazi mbele zake). Ukumbuke ni watu waliofanya vitu kwa kuangalia uhitaji wa watu kwamba sasa wanahitaji kucheka kwahiyo nifanye hivi ili wacheke, nawakati huu ninahitaji nifanye kitu fulani ili wanione kwamba niko namna gani (wakati huo unafanya hujui unaharibu C.V yako kwa watu) ila tu siku zote ukumbuke kuwa kuna C.V aina mbili 1: C.V unayoiandika kwajili ya application za kazi. 2:C.V unayoitengeneza vichwani mwa watu. Sasa unapoziandaa hizi C.V zote mbili kuwa makini ili usije ukaharibu hata mojawapo.

Wale wasomi unaowafahamu wako nyumbani, wanauza soksi, barafu, na ice cream, lakini wanashahada, stashada zao nzuri na matokeo mazuuri, lakini wako pale kwa sababu, ya uzembe fulani walioufanya wakati wako chuoni kama wewe hapo kwa vile unavyo vifanya, kosa lililofanyika ni *kutojitambua mapema* na wengi wanajikuta wanajitambua wakati wameshatoka masomoni, na kukaa muda mwingi nyumbani na wakati huo walikwisha kupoteza fulsa walizokuwanazo mapema na kufanya vitu kwa kuhofia wengine na kujisahau wao.

Ni heri usifanye chochote leoukaanza kufanya kesho kwa kujipunguzia lawama kwenye kesho yako, lakini wakati huohuo uwe makini kwenye mambo yako yakae sawa

kulikokukaa bila chochote, mwisho wa yote ukaumbuka kwa kujikuta wewe si chochote, lakini kitu natamani ukifanye ni kitu kitakachoingiza faida kwako kiuchumi, usifanye vitu vya kudhalilisha utu wako.

*"Usipojua wewe ni nani, ni heri kutikufanya chochote, kuliko kufanya chochote ukajilaumu kesho."* Nikiwa na maana kuwa ukifanya vitu bila kujitambua ni hatari kwako, kwa sababu, nichukue mfano kuwa wewe ( yule wa ndani) ni Raisi wa nchi au kiongozi , lakini bado hujajitambua kuwa unatakiwa kubeba nafasi gani, ukaanza kuiba, ukawa tapeli,fisadi,ukafanaya ukatiri mabimbali, ukapata mashutumu mengi,ukashtakiwa na kufunguliwa failizakesimbalimbali zenye uthibitisho, ukapata hukumu ya jaji, ukapita jera na baadae baada yakutoka jera ukakaa na kujiuliza hivi mimi ni nani? Na ukajua wewe ni Raisi, ukataka kuanza harakati za kuwania nafasi za uongozi na lengo lako ufikie nafasi ya uraisi,kwa sababu ya shutuma zote ulizozifanya na kesi zilizoko mahakamani, unakuwa umepoteza vigezo vya kuwania hii nafasi na kuwa Raisi wa nchi. Kinachobaki hapa ni lawama, kujilaumu kwanini nilifanya haya, kama ulifanya kwa msukumo wa marafiki, utalaumu kwanini niliwapokea hawa kwenye maisha yangu,nikawapa nafasi ya kunifundisha wanachokitaka, na ndio wakati ambao yule mtu wa ndani anaanza kukupatia adhab ya siku zote.

Au mdada ukahangaika na uasherati wakati wa masomo ukapata mimba na kufanya abortion, ukasahau kuwa WEWE NI MAMA ikafikia hatua ambayo umepoteza uwezo wa kushika mimba , ukajisenea moyoni sasa natakiwa kuwa mke wa mtu na niwe na familia, ukaingia kwenye ndoa lakini sikuzote usipate mtoto, baadaye ukatafakari na kukumbuka njia zako wakati wa ujana, unaaza kulaumu na kuumia siku zote. Lakini katika yote ni kwa sababu ya kuto kutambua nafasiyakokwabaadaye au kutambua nafasi yako ya baadaye lakini kiuto kuona thamani yake zaidi ya vitu unavyovifaya kwa sasa, nikupejambo moja hapa kwamba *mambo mengi yanayoharibu uhalisia wako ukiyafanya ni mazuri na yanafurahisha lakini kwa upande wa pili huwa yanakung`ong`a.*

Sikuzote chunga tabia zako, na ufanye vitu kwa kutoa mihemko yako pembeni ili vyema na kabra ya kufanya jambo make sure you ask yourself following question,

What to do? Now you should to discover the things to do.

When to do? Your needed to state good and specific time to implement the goal.

Whom one I need to do with? Your needed to find out someone who can help you, who can promote you, who can advice you, who can tell you the truth.

Why I want to do it? The reason to do, now you need to evaluate the positive result and negative result. This place your needed to be careful because is the place to approve goal if it is productive or not.

Where to do? Decide the place which your goal will be carried out, ni jambo la muhimu

sana kujua utafanyia wapi jambolako, na pale unapohitaji uwepo wa watu iwe rahisi kutoa direction, lakini pia ukichagua eneo mapema nirahisi kupata ushauri kuwa eneo linafaa au halifai.

After asking those these question , I can allow you to do what you want to do, according to good answer you give yourself, if you don`t get reasonable answer please find out someone else who can advice you.

Katika yote unatakiwa kujua unafanya nini, kwa wakati gani, na unaleta impact gani kwako wewe (mtu wa ndani/ uharisia wako)

## NIFANYE NINI KAMA NINAISHI AMBAYE SIO MIMI?.

Unajiuliza hili swali baada ya kujua wewe ni nani na unatakiwa kufanya nini, lakini kwa sasa unasomea kada ambayo haikupeleki au product yake haimfanyi yule ambaye ni wewe ( yule wa ndani). Kwa bahati mbaya wengi wakijua hilo, huwa wanaanza kufanya vitu vya ovyo, wkati mwingine wanaanza kuishi ilimladi, wanaonekana wako vyuoni kwa kuhofia kurudi nyumbani pasipo sababu za msingi, huwa wanaamua kubeba ule msemo unaosema chuo bata na kuanza kuishi huo msemo, wakati huo wanaanza kutoka zaidi, toka walipokuwa na kwenda mbali zaidi, yaani nikama ulitolewa nje ya njia na baada ya kujua kuwa uko nje ya njia, ndio unaenda mbali zaidi , yaani msituni na baada ya kupotea huko ukapata matatizo ndipo unaanza kutafuta njia, wakati huo utasumbuka sana kupata njia sahihi kwa sababu kila njia utakayokutananayo utaona ni sahihi na inakufaa wakati huo njia hiyo haikuhusu na unaendelea kujichelewesha na kupotea kabisa.

Hatakama utakuwa umegundua kuwa course unayoisoma haitakufanya kuwa wewe (yule wa ndani), basi tafuta fulsa mbalimbali kwenye mazingira uliyopo zinazoweza kumtengeneza yule ambaye ni wewe( yule wa ndani), huku ukiendelea na masomo, wakati huo ukipiga hesabu mpya kwamba baada ya kuhitimu course uliyopo, unaenda kufanya application za course itakayo sababisha uweze kumfanya yule ambaye ni wewe (yule wa ndani) na ukikusanya information mbalimbali na ujuzi kuhusu course husika, sio kufanya usumbufu kwenye course usiyoipenda, maana unapofikiri kuwa usumbufu ndio njia ya njema ndio wakati unaoutumia kumharibu yule ambaye ni wewe (yule wa ndani), na pia kuharibu CV yako kwa watu, maana watu husema *tunasoma na mabosi.* Fanya vitu kwa hekima ujitunze.

Tulia masomoni maliza hapo ulipo ndipouanze kumtengeneza yule ambaye ni wewe 9yule wa ndani ), na kama unafulsa ndani ya masomo , soma hukuukiendelea kutumia fulsa, lakini pia ukijitahidi kusoma na kumtengeneza yule ambaye ni wewe ( yule wandani ).

## [illegible] NIWE WA KIPEKEE?

Ukae ukijizungumzia wewe na kutafakari kwa upana ni tabisa gani ukonayo na unaionyesha ndaniya jamii, na kukupa upekee wako, yaani sifa za namna yako.

Unajua sikuzote watu hutamani mtu wa tofauti au bidhaa ya tofauti yenye sifa za kipekee wake, maana ule upekee ndio unaoifanya bidhaa ile, ionekane bora kuliko zingine, au naweza kukuuliza wewe ni specialist kwenye sifa zipi? Kama hiyo sifa inauwezo wa kutumika ili uweze kumtengeneza yule ambaye ni wewe,itumie ikutengeneze lakini kama haupo kwenye uharisia wakwako au tabia ulizonazo siosahihi hutafikia hatima njema.

## [illegible] KULIHUDUMIA?

Unatakiwa kutafuta kundi ambalo ukilipatia huduma yako litafaidika na huduma yako lakini wewe ukiwa kwenye process ya kumtengeneza ambaye ni wewe ( yule wa ndani ).

Muda ule nilipo jitambua ilinibidi kujiuliza je nikundi gani ninalotakiwa kulihudumia, na kuwapa kitu nilichonacho wakafaidika na mimi nikiwa na mtengeneza yule ambaye ni mimi ( yule wa ndani), now I have come to realize kuwa ninamakundi matatu ambayo ni 1. Vijana wa kikristo na wasio wa kristo. 2. Wkristo 3. Jamii ya watu ( watu wazima). Kwenye kundi la vijana nikagundua nina kundi la wanavyuo pia ambao nivijana almost,kwahiyo nimeingia chuoni nikaanza kuishi maisha yangu ya kawaida kama wengine wanavyoishi, lakini pia nikichunguza ni namna gani watu huyachukulia maisha ya chuo nikagundua kuwa jamii inaelewa mtu akienda chuo lazima atakuwa ameharibika,sasa ili  bidi kutafuta njia kadhaa za kujaribu kuwabadirisha ndipo nikapata heading ya hii kazi.

Paleunapojua kuwa  ni kundi lipi, unalotakiwa kulihudumia lazimautoe muda wa kuchunguza vizuri ili ujue linahitaji kitu gani?, linaishije?, namna gani utafanya ili likukubali kupata huduma kwako?, je ni hudumagani utaitoa kwao na wataikubali?.

## [illegible] WANAOKUTEGEMEA?

Tukiachana na ile hali unafikiriaga kuwa unatafuta maisha kwaajiri yako, unajilisha upepo,ukifikiria kuna mkeo/ mumeo, watoto wako, wakati mwingine ni wadogozako na wazazi,ni watu ambao unatakiwa kujua kabisa wanakutegemea au watakutegemea, na usipo kaa sawa kwa sasa ukasema nitakamilisha mambo yangu kadiri muda unavyoenda, utajikuta unaishia kwenye majukumu na hata sikumoja hutafikiria tena

kuwa kuna habari za kuwa wewe ( yule wa ndani).

Ukijua ni nani na nani wanakutegemea na ukaonaumuhimu wao japo huwaoni au unawaona, hufahamu ni wangapi, huwezi kufanya ujinga pale unapofanya mchakato wa kumtengeneza yule ambaye ni wewe ( mtu wa ndani ),hapa ndipo unaanza kuona mtu anasema nitakuwa na watoto wane,ili nianze kutengeneza uwezo  wa kufanya management ya watu sita, na huwa atakuwa serious kufanya kitu anachokifanya ili aweze kufikia hatua ya  kumfanya yule ambaye ni yeye (yule wa ndani), lakini tunakuwa nawatu ambao mpaka unafika muda wa kuoa na kuolewa hajui atakuwa na watoto wangapi, ndipo tunapoanza kuona zile familia zaenye watoto kumi na mbili na wakati huo mzazi anauwezowa kulea watoto wawili, kwahiyo hao wengine kumi wamekuja kuteseka tu,na baada ya muda tunaanza kuona hao kumi wanaanza kufanyiwa mgawanyo wa kwenda kwa ndugu na jamaa, ambapo hujui nani anaenda kufanya nini huko anakoenda maana watu huwa tunatofautiana kunamwingine atawapokea vema mwingine atawapokea tu kwasababu ninduguyo lakini kifuatacho chuu ya mtoto wako hakielezeki, ndiomaana sehemu zingine kunasheria ya kuzaa watoto mwisho idadi kadhaa,hiyo yote walikuwa wanajaribu kupunguza matatizo ya namna hii, kama watu hawatakaa kutathmini idadi ya watoto watakao kuwa nao basi mamlaka inachukua jukumu la kupanga kwa niaba yao.

Kwa hiyo kaa tathmini ni watu gani na niwangapi wanao kutegemea, kisha upange vyema maisha yako namna yatavyokuwa na jinsi utakavyo yaendesha wakati huo ukimtengeneza yule ambaye ni wewe(yule wa ndani) ili unapofika wakati wa majukumu, uwena focus ya jambo moja